

Nafasi Ya Fasihi Simulizi Katika Kuwasilisha Ujumbe Kisheria: Mfano wa Uendeshaji Kesi Za Kitamaduni Miiongoni Mwa Babukusu.

Ikisiri

Utafiti

uliazimia kubainisha nafasi ya Fasihi Simulizi katika kuwasilisha ujumbe kisheria. Ulionyesha namna
vipengele bainifu vya Fasihi Simulizi vinaweza kutumika kuwasilisha ujumbe kisheria. Ulifanya hivyo kwa
kuegemea uendeshaji wa kesi kitamaduni miiongoni mwa
jamii ya Babukusu. Ili kuafikia lengo hili utafiti
ulitumia mbinu ya kithamano. Idadi lengwa ya utafiti ilikuwa jumla ya kesi
za kitamaduni tulizohudhuria na
kuzirekodi. Utafiti ulijumuisha mbinu ya uteuzi wa sampuli kimaksudi.
Uteuzi wa sampuli kimaksudi
ulitumiwa
kuchagua Chifu, naibu wa Chifu, mwenyekiti wa baraza la wazee na
makala maalum yaliyoandikwa kuhusu
Fasihi Simulizi na Sheria. Nao uteuzi wa sampuli kinasibu ulitumiwa kuteua
mabaraza ya wazee na ya Chifu
tuliohudhuria. Waaidha, uchunguzi ulihusi
sha mbinu za uchambuzi wa yaliyomo, usaili na uchunzaji
-

shiriki.

Njia hizi zilitumika kukusanya data nyanjani na maktabani. Matokeo ya
utafiti yalichanganuliwa kithamano.

Hii ni mbinu ya kuchanganua data ambayo mtafiti anaeleza na kufafanua
matokeo ya utaf
iti wake kimaelezo.

Uchunguzi huu vilevile uliongozwa na nadharia ya Mwingilianomatini.
Kwa mujibu wa kesi tulizohudhuria,
utafiti ulibaini kuwa kuna vipengele vya Fasihi Simulizi ambavyo
vinaoana na hali ilivyo katika taaluma ya
Sheria wakati wa uendeshaj
kesi kitamaduni miiongoni mwa jamii ya Babukusu. Kwa hivyo ni muhali
kusema

kuwa matini za Kifasihi Simulizi huwa zinachota, kunukuu, kugeuza, kuiga kwa namna ya kufumba, kubeza au kurejelea kwa njia moja ama nyingine matini za Kisheria. Hali kadhalika tan zu zenyewe za Fasihi Simulizi zinaingiliana na kuchangiana katika kutimiza mahitaji ya jamii kuitia shughuli mbalimbali.

Waandishi

Winnie Musailo Wekesa, Fred Wanjala Simiyu, Opande
Nilson Isaac